FURSA ZA UTALII KATIKA WILAYA YA PANGANI

S/N	VIVUTIO VYA UTALII	SHUGHULI
1	**BAHARI YA HINDI NA FUKWE** 	1. Bahari ya Hindi ambayo iko kwenye Pwani yote ya Wilaya ya Pangani, maeneo ya fukwe na ukanda wa Pwani yanaweza kupanua wigo wa biashara ya utalii wenye kuhusisha utalii wa kiutamaduni na mazingira katika kupumzika ufukweni, kucheza Michezo mbalimbali ya Baharini- Kupiga mbizi, kuzamia, kuogelea, Uvuvi wa mashindano, kulala mchangani, mashindano ya mbio za ngarawa na mashua, kupiga picha, kufanya pikiniki, kutokana kwamba tunazo fukwe nzuri zenye mchanga msafi usio na tope. Kutembea masafa mafupi na marefu na kubarizi upepo mwanana., Uvuvi wa kienyeji kwa ngarawa, uvuvi wa kibiashara ili kutosheleza soko la ndani na nje. Kilimo cha cha Bahari-mwani, Mahoteli mengi yanahitaji samaki wa kutosha kwa ajili ya watalii wanaofika Pangani. 2. *KISIWA CHA HIFADHI YA MAZIWE*- Kuangalia Kasa wa kijani wanapokuja kutaga, Kupiga Mbizi, Kuogelea, Kupiga Picha, kulala mchangani, Kuona Nguva, kuona samaki aina aina, kuona maisha na ekologia ya bahari, matumbawe, Kufanya utafiti, kuona kasa wa kijani wakija kutaga wakati wa msimu. Usafirishaji wa Watalii kwenda Kisiwani huongeza kipato kwa Serikali na wananchi. Hivyo ulinzi wa kisiwa hiki ni muhimu sana.

1.	**KUTEMBELEA MJI MKONGWE WA PANGANI** 	Kwa kutumia Waongozaji watalii wenye ujuzi wa kazi hii kutoka kwenye Kituo cha Utalii Pangani, wataweza kuonyesha watalii wa nje na ndani, maeneo a Kihistoria ya mji mkongwe wa Pangani, Ukuta wa bahari, Minara ya makumbusho, majengo ya kihistoria ujenzi wa mawe na chokaa, Pangani na Bweni,yenye nakshi na milango ya kuvutia, misikiti, Uwanja waUhuru, magofu na makaburi ya chimbuko la mji wa Pangani ya Mhembo, Kumba, Bweni. Na Miji mingine maarufu ya kale ya Ushongo, Kipumbwi, Mkwaja na Buyuni. Halmahsauri iliunda kikosi kazi chini ya idara ya Maliasili na Utalii PCCTP ikiwa mmoja wa wajumbe na msimamizi akiwa UIKWASA na kwa Msaada wa Idara ya Mambo ya kale na wafadhili, majengo matatu yamefanyiwa ukarabati wa dharura. Wakazi wa Mjini waendelee kuhamasishwa iki kulinda hii mali kale ambayo ni urithi wa kizazi kijacho.
11 1.	**KUTEMBELEA MIRADI YA KILIMO NA MAZINGIRA** 	Kutembelea mashamba ya Mkonge na kuona mkonge ulioletwa na Mjerumani Bwana Richard Hindroph mwaka 1892 kutoka Yukatani Amerika ya kati na kuupanda kwa mara ya kwanza kule Kikokwe –Pangani. Mmea huu hutoa kamba za matumizi mabalimbali na mbegu zake zinaota juu ya mlingoti, Mtalii pia anaweza kuona Mipopoo, minazi na kunywa kijinywaji safi cha madafu, Kuona mazao anuwai ya biashara na chakula. Miradi ya kuhifadhi mazingira, Mbogamboga matunda, na wanyama wafugwao. Kutokana na wilaya ya Pangani kuwa na rutuba ya kutosha, wananchi wana nafasi kubwa kuinua soko la utalii.

1 V	**MTO PANGANI**  	Mto maarufu wa Pangani ambao maji yake yanatoka kwenye mlima mrefu Barani Afrika. Ni mto peekee wenye maji safi unaongiza maji yake kwenye Bahari ya Hindi, na chimbuko la Umeme wa Maji kutoka Hale.Watalii hupenda kusafirishwa kwa mashua na kuona uoto wa mikoko, ndege wa ainaaina, wanyama wadogo kama kima, tumbili mbega na wanyama wakubwa kama Mamba, Viboko, Samaki , kamba, ufugaji wa kaa kwenye mikoko ambayo ina ikolojia ya pekee. Ya mazalia ya viumbe hawa na uvuvi wa asilli.
V	**KUTEMBELEA MISITU YA HIFADHI** 	Wilaya ya Pangani ina misitu mingi ya asili na misitu ya kupandwa iliyoko kwenye uangalizi wa serikali katika ngazi zote na misitu mipya inayoendelea kupandwa na Kampuni ya misitu iitwayo Tanga Forest. Watalii wanaweza kutembelea misitu hii ili kuona miti, ndege mbalimbali, vipepeo, wadudu na wanyama. Baadhi ya misitu hiyo ni Msubugwe,– Tarafa ya Mwera Misitu ya Mikoko kando kando ya bahari na maingilio ya mito, Msitu wa hifadhi wa Garafuno –Tarafa ya Mwera, Gendagenda Kaskazini – Tarafa ya Mwera, Msitu wa Kibubu – Tarafa ya Madanga Mradi wa Misitu- Tanga Forest Project Mtango, nk. **Picha ya mikoko, mnazi//////////////////////////**

V 1	**HIFADHI YA TAIFA YA SAADANI** 	Hifadhi ya Taifa ya Saadani iko kusini ambapo inapakana na Wilaya ya Bagamoyo. Makao makuu ya Hifadhi hii yako katika wilaya ya Pangani kule Mkwaja. Mto unaofanya mpaka uko karibu na katikati ya hifadhi ambao unaitwa Mligaji. Kuna miti mingi y miombo, migungana mikoko inayoota kwenye mito iingiayo baharini. Watalii wanaweza kupelekwa na waongozaji watalii na kule hifadhini watapokelewa na Mabwana Nyama waongozaji watalii wenye ujuzi mkubwa. Yapo mahoteli ya Kuvutia kando na ndani ya hifadhi hii. Wanyama wengi wa aina mbali mabali wako hifadhini kama Simba,Tembo, chui,nyani, punda milia, Nyati, nyoka, vipepeo ,nyuki na mji mkongwe wa Saadani. ndege wa aina mbalimbali, Kasa wa Kijani kwenye mazalia ya kasa kule Madete. Ni Hifadhi pekee ambayo watalii huweza kufurahia kuona Maisha ya Bahari na Mbuga za wanyama.
V 1 1	**UUZAJI W A SANAA ZA UFUNDI**  	Wenyeji wa Pangani ni Mafundi mahiri wa utengenezaji wa bidhaa za Sanaa za ufundi kv. Uchongaji, uchoraji, usukaji wa mikeka , majamvi, miswala, ufinyanzi. Urembo wanguo,batiki. Shanga nk Kuna umuhimu wa Kuanzisha Sakosi za Viwanda vya Sanaa na wasanii kupata mafunzo ya ujasiliamali na utengenezaji wa Sanaa bora ikizingatiwa kwamba Katika mji wa Pangani, hakuna duka la sanaa. Hoteli za Kitalii zina maduka machache ya kuuzia bidhaa hizi kwa Watalii. Pia kuna umuhimu wa kutangaza Sanaa zetu nchi za nje na kupanua masoko.

VIII	**UUZAJI WA BIDHAA ZA KILIMO NA UFUGAJI** 	Kushiriki Katika Uzalishaji Wa Bidhaa za Kilimo Ili Kutosheleza Soko na Mahitaji ya ndani ya Wilaya Kv Mbogamboga- Nyanya, Vitunguu, Bamia, Biringanyi, Mchicha, Matunda, Ndizi. Ufugaji wa kaa, ufugaji wa kuku, uuzaji wa mayai,, ufugaji wa nyuki ili kujitosheleza na asali, wang'ombe ili kupata maziwa. nk. Vukundi viwezeshwe ili vizalishe bidhaa bora zinazoweza kuuzwa kwenye mahoteli yetu ya Kitalii ya Pangani.
IX	**UKARIMU WA WENYEJI NA HUDUMA ZA MAMA LISHE.** 	Wenyeji wa Pangani ni wakarimu sana. Vilevile wanafahamu mapishi ya aina mbalimbali ya vyakula vya kienyeji. Wanaweza kupika mchele kwa mitindo tofauti tofauti, na pia kupika Chai yenye viungo na vitafunio vya kila aina.. Wakidhamiria kukupikia hayo madikodiko, utasahau. Mapishi ya Samaki, hapa umefika. Samaki wa kupaka, kukaanga, wa mchuzi na mambo ya aina hiyo. Ziko pia aina tofauti za mapishi, mbogamboga na kila mlo utapambwa na matunda bila kusahau mapishi ya ndizi na muhogo. Katika vijiji vya Mwambao ambako kuna uwezekano wa kufikiwa na wageni, kuna umuhimu wa Kuendeleza vikundi 22 vilivoorodheshwa, ili kupata mafunzo ya Maandalizi bora ya Vyakula, uhifadhi na usafi wa vyakula, kuandaa meza nk. Shirika letu la Utalii limetoa mikopo ya ST-EP kwa baadhi ya vikundi. Watalii pia wanaweza kukaribishwa majumbani na kuishi na wenyeji wao,kutia hina na wanja, kusuka nywele, kuangalia ngoma za kienyeji. Kwa kufanya hivyo, ndipo, watalii wageni wanaweza kufaidi utalii wa kiutamaduni. Tunapaswa kuthubutu ili kupiga vita umaskini kwani fursa tulizo nazo zinatosheleza kubadilisha hali ya maisha yetu kiuchumi na kuondoa umaskini kama tutaziboresha.

XI	**UTAFITI NA HUDUMA ZA WAGANGA WA JADI**	Watalii wengi na wanafuzi wanapenda kutembelea na kupata maelezo ya kisayansi ya Tiba za Jadi. Kuna umuhimu wa kendeleza waganga hawa ili kazi zao ziweze kupata mshiko wa utafiti wa kisayansi kwa manufaa ya vizazi vijavyo.
XI	**BURDANI ZA SANAA ZA MAONYESHO- NGOMA, MAIGIZO, MUZIKI WA JADI**	Wasanii wetu maarufu hapa Wilayani wamekuwa mahiri sana katika fani hii na watali wamekuwa wakiandaliwa vikundi hivi kupata burdani ya pekee yenye vionjo sahihi vya Kiutamaduni. Kuna haja ya kuviendeleza vijundi hivi hasa katika sanaa za kiishara (mime) ili waweze kufikisha ujumbe kwa wepesi zaidi kwa watalii wetu. Watalii wanaweza pia kupiga picha wakati wa shuguli hizi.
XII	**USAFIRISHAJI WATALII BAHARINI NA NCHI KAVU**	Kuwa na usafiri wa uhakika wa usafirishaji wa watalii kwenda Zanzibari kwa kutumia boti za kuaminika na vifaa vya usalama. Vilevile, kuanzisha makampuni ya usafirishaji ndani na nje ya Wilaya kv. Tongoni, Tanga, Amani nk. Rai yetu ni kwamba, wenyeji sasa wahamasihwe na kuwezeshwa ili washiriki katika biashara ya Usafirishaji wa Watalii majini na nchi kavu...

CHANGAMOTO:

Kutokana na kuwepo na msukumo mkubwa wa kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyoko katika Wilaya ya Pangani pamoja na fursa zilizotajwa juu, sekta ya utalii inaweza kuwa chanzo kikubwa cha kuchangia uchumi kwa jamii ya wananchi ili kuondoa umaskini. Wilaya ya Pangani ina Fukwe zenye Mahoteli mengi mazuri ya Kitalii ambayo mwaka 2008 walipokea watalii wastani wa 12,000 ambao waliweza kukaa Pangani kwa wastani wa siku 3 kutokana na ukosefu wa Intaneti pekee. Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

1. Uhaba wa Waongozaji na watembezaji watalii wa kutosha wenye ujuzi.Tuna vikundi kutoka Pangani,Ushongo, Mkwaja, Buyuni na jirani zetu wa Saadani, ambao wanatakiwa kupatiwa mafunzo zaidi ya taaluma hii changamoto kubwa katika sekta hii ni kutojua lugha ya Kingereza vizuri ambayo ndio njia ya mawasiliano ya kimataifa.
2. Mama lishe wenye ujuzi wa kupikia na kukaribisha watalii kutoka kwenye vijiji vya mwambao vyenye uwezekano wa kutembembelewa na Watalii. Wanatakiwa kuendelezwa kitaaluma ili waweze kutoa huduma bora.
3. Usafi wa mazingira na Fukwe. Uwe ni jukumu la watu wote na si mwambao tu, hata mazingira ya nyumbani kwakuwa uchafu hauambatani na ustaarabu.Wananchi wote waepuke kuchafua bahari kwa mifuko na chupa za plastiki au sandarusi
4. Uharibifu wa mazingira malikale na uharibifu wa mikoko.
5. Wawekezaji kuitangaza Pangani na Saadani kama kivutio cha Pekee chenye mbuga za wanyama wanaofika ufukweni, na Kasa wa Kijani.
6. Kuendeleza wavuvi kwa kuwapatia mafunzo na uvuvi bora na kuzingatia sheria kwa manufaa yao na vizazi vijavyo.
7. Ulinzi wa shirikishi wa kisiwa cha Maziwe na kuona uwezekano wa kurejesha uoto wa asili. na kuhakikisha kuwa inalindwa ili kuepuka kabisa uvuvi haramu. ili kutunza aina mbalimbali za samaki wenye soko zuri lenye tija kwa wenyeji nakukuza utalii. Ni vema mamlaka kuweka mipaka ya kueleweka pale kisiwani.

Imetayarishwa na. kuwasilishwa na: Leonard A.Sekibaha
Mratibu, Pangani Coast Cultural Tourism Programme.
22nd, July 2009.